




Kwa heshima ya:

Wale wote ambao wamejikuta wanapenda tena

May 17, 2010

JUMATATU

Niliondoka nyumbani kwenye majira ya saa tatu za asubuhi nikisindikizwa na jua kali la asubuhi lililofanya anga la Dar kama mbingu iliyofunguliwa na kuruhusu neema na baraka ya joto itawale. Kwa kweli sikuwa mpenzi wa kwenda katikati ya Jiji la Dar hasa katikati ya wiki. Mara nyingi wanaofanya hivyo ni dereva wangu au wasaidizi wengine wa hapo nyumbani. Ni wao ndio wanaenda karibu kila siku kufanya manunuzi mbalimbali ya mahitaji ya hapa nyumbani na kufanya shughuli mbalimbali ambazo mzee au mimi nimewaagiza.

Jumatatu hiyo nilikuwa nimekwishawatuma vijana kwenda mjini kufanya shughuli mbalimbali ndipo nilipokumbuka kuwa nilitakiwa kwenda kwenye ofisi ya Ardhi kufuatilia vibali vya viwanja vyetu vipya vya huko Kunduchi. Hilo lilikuwa linanihitaji mimi mwenyewe kwenda na si mtu mwingine. Pamoja na kuwa na chuki ya kuendesha gari jijini Dar nilijilazimisha kuondoka nyumbani asubuhi hiyo nikiwa na dhamira ya kurudi mapema sana iwezekanavyo nikimaliza tu shughuli zangu mjini. sikutaka msongamano wa jiji la Dar unikute niko mjini kwani kati ya vitu vingi ambavyo vimenishinda kabisa ni hilo la kukaa foleni masaa kwa masaa..

Nilipiga ufunguo gari langu la Mercedes ML350 la rangi nyekundu na taratibu nilianza kukanyaga mafuta nikitokea nyumbani maeneo ya Kiluvya kama dakika kumi na tano hivi kutoka Mbezi Mwisho. Kwenye barabara hiyo ya vumbi nilianza kwenda taratibu huku nikiwapita waendesha baskeli kadhaa na wanakijiji wengine ambao walikuwa wanatoka au wanakwenda kituo cha basi. Nilikuwa naburudishwa taratibu na nyimbo za nyimbo za dini kutoka Radio Maria kwani nilipojaribu kusikiliza kile kituo kingine cha radio maarufu nilijisikia kuumwa na kichwa. Mawazo yangu yalikuwa kwenye mambo elfu moja na moja, nikipanga na kupangua, nikikadiria na kukagua mahesabu huku nikijaribu kufanya mikakati mbalimbali ya kutatua matatizo ya hapa na pale ya nyumbani na ya biashara. Kwa kweli wakati mwingine nilijisikia kuchoka na kuzidiwa na mambo. Hata hivyo niliyapenda maisha yangu hivyo.

Utaniwia radhi sijakuambia jina langu; ninaitwa Clementina na ni mke wa Waziri mmoja katika serikali yetu hii; kwa wakati huu naomba nisitaje jina lake wala wizara anayoiongoza maana unajua tena waswahili hawachelewi.

Tumekuwa katika maisha ya ndoa kwa miaka kumi na tano sasa na tumejaliwa watoto wawili, wa kiume na wa kike. Wakike Renata ndio ameenda kuanza kitato cha kwanza huko Kifungilo mwaka huu na wa kiume Renatus anasoma mojawapo ya International Schools zetu hapa hapa Jijini Dar. Kuteuliwa kwa mume wangu kuwa Waziri kuliwashangaza watu wengi lakini kwa wale wanaomfahamu i Mume wangu amezama katika mambo yake ya siasa na hasa wakati huu mambo ya uchaguzi yakiwa yamepamba moto. Mimi nimebanwa zaidi na shughuli za kusimamia miradi yetu mbalimbali iliyotapakaa sehemu mbalimbali nchini. Wenyewe wananiita (na ndivyo nilivyo) mfanyabiashara. Siasa siipendi wala siitamani. Wengi hawalijui jina langu zaidi ya kuniita “mke wa waziri”!

Nilifika katikati ya jiji karibu masaa matatu baadaye na sikupoteza muda kwani sikuwa na kusudio lolote la kuwa huko muda zaidi ya kile kilichonileta. Niliegesha gari langu kwenye maegesho ya Wizara ya mume wangu ambako si mbali sana na ofisi za Ardhi. Kwa kawaida ninapokuwa mjini huwa naegesha hapo kwani wananifahamu na kuna usalama wa kutosha tu. Sikutaka kuingia Wizarani kwani sikuwa na sababu yoyote ya kufanya hivyo. Kwa sababu za kiusalama hata hivyo Mzee Yusuph ambaye ni mmoja walinzi pale (Mzee ni jina lake la kwanza licha ya kwamba ni kweli ni mzee wa makamo kidogo) alifuatana nami kuelekea Ardhi. Huwa anafanya hivyo mara nyingi ninapokuwa mjini na kama si yeye basi anamuagiza mlinzi mwingine kufanya hivyo. Mwenyewe nafurahia yeye anapojitolewa kwani ni mcheshi na huwa ananipa kampani nzuri.

Tukiwa tunaelekea Ofisi ya Ardhi Mzee Yusuph alikuwa ananipa michapo ya mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye familia yake, vituko vya hapo wizarani na kila aina ya stori ili kuharakisha safari yetu hiyo fupi. Mimi nilikuwa msikilizaji na mdadisi wa hapa na pale. Kwa kweli alikuwa ni chanzo kizurbi cha habari za ukweli, umbea na hata zile za kutokuaminika kabisa. Nakumbuka alinisimulia kuwa yule mtu aliyeota manyoya alichukuliwa na Wamarekani kwa uchunguzi ndio maana serikali

ilifanya haraka kukanusha.

Dakika chache baadaye tulifika Ofisi za Ardhi na sikupoteza muda mwingi nilienda kuonana na niliokusudia kuwaona na, wakati huo mzee Yusuph alikuwa nje ananisubiri huku akivuta sigara yake na kupuliza moshi utadhani gari moshi lililofika kituoni. Nilipokamilisha mambo yangu ilikuwa karibu saa nane za mchana; nilijisikia ahueni na mwenye furaha. Nilijua hatimaye mambo ya ujenzi ambayo yalikuwa yamechelewa kule Kunduchi yataanza muda si mrefu. Mradi wetu wa Kunduchi ndio utakuwa mradi mkubwa katika orodha ya miradi yetu.

Tulianza taratibu msafara wa kurudi kuelekea Wizarani huku mzee Yusuph akinisimulia kisa cha jamaa mmoja aliyeibuka siku za karibuni anaitwa Nabii Tito. Sijui kama ni kisa cha kweli lakini kwa mujibu wa Mzee Yusuph huyo Nabii anajua “sana” Biblia na amekuwa akidai kuwa Pombe ni dawa ya Ukimwi na madai mengine mbalimbali ambayo hakuna mtu ameweza kuyapinga kwa kutumia hiyo Biblia. Mimi nilibakia kucheka tu kwani simulizi hilo lilikuwa ni kama hadithi za kufikirika tu na burudani.

Nilijikuta nacheka hadi nashindwa kubania na mtu mwingine ambaye asingeweza kutujua angeweza kufikiria mzee huyo ananiimbisha na mimi naingia laini taratibu. Tuliendelea taratibu huko mzee Yusuph akinionesha baadhi ya mabadiliko ambayo nimeyamiss mjini hapo na vituko vya wanasiasa wa nchi yetu ambavyo alikuwa anavisimulia utadhani alikuwa ni shahidi wa kwanza mahakamani. Kwa kweli siku hiyo imeenda vizuri kabisa; nilifurahia kuwa na mzee Yusuph pembeni. Hakuniboa.

Mawazo yangu hayo na vicheko tulivyopokezana na mzee huyo mcheshi vilitibuliwa tulipokuwa umbali si mrefu kutoka jengo la Wizara tulikokuwa tunaenda. Mzee Yusuph alikuwa amenielekeza kuangalia jengo moja jipya ambalo lilikuwa linadaiwa ni “la Fisadi Supremo” ambaye ni kigogo mmoja wa CCM. Lilikuwa jengo zuri kwa nje na lingeweza kuwepo kwa jiji lolote maarufu duniani. Jengo lile lilinivutia sana na katika kuangalia sikuwa naangalia ninakokwenda.

Kilichonishtua na kunirudishia fahamu ni mgongano wa kihistoria, mgongano wa kukumbukwa, mgongano wa miili ya watu wawili ambao ungeweza kabisa kutoa cheche! Kama gari bovu lililogongana na treni lililosimama nilijikuta nimemvaa kijana mfanyabishara ambaye alikuwa amejisimamia nje ya kibanda chaka akipiga soga na wenzake. Sijui kama nilimgonga au alinigonga (kwa lengo la mjadala huu tukubaliane alinigonga) lakini mimi ndiyo niliathirika zaidi kwani nilisikia hadi kizunguzungu. Maumivu kifuani niliyasikia hadi kwenye ulimi.

Mkoba wangu niliokuwa nimebeba nyaraka mbalimbali ulianguka pembeni na mzee Yusuph ailifanya hima kuuokota. Yule kijana kabla ya kugongana na mimi alikuwa anakunywa juisi katika gilasi na ule mgongano ulisababisha juisi yote inimwagikie kifuani utadhani ilikuwa ya kisasi. Ubaridi wake ulipenya taratibu kwenye nguo zangu kuanzia blauzi hadi sidiria na kugusa ngozi yangu katika hali ya kunifanya nikereke. Nilishikwa na hasira. Niliyumba kidogo na kama isingekuwa mzee Yusuph kunidaka nina uhakika ningepiga mweleka chini mchana kweupe! Nina uhakika magazeti ya udaku yasingechelewa kutangaza “mke wa Waziri ajiachia!”

“Sorry, Sorry mama, I’m really sorry” alianza kusema huku mikono yake ikiwa imeinuliwa kuniomba radhi. Akinyosha mikono hiyo kama kunishika lakin bila kunigusa. Alikuwa anatetemeka. Matumizi hayo ya kiingereza na lafudhi yake utadhani mjamaika ilinichafua zaidi. Hadi *Wajamaica wameingia bongo?*

“Wewe vipi! Huangalii unakokwenda?” nilianza kumfokea. Sikujali kama lilikuwa ni kosa langu au la; mimi mke wa Waziri ati!

“Sorry, I didn’t see you madam” akasema tena kwa kiingereza chake cha Ki-jah people! Alizidi *kunitibua.*

“We umetoka wapi! Yaani huangalii barabarani, mjini hapa usilete mambo ya kishambakishamba” nilianza kumpaka; nilijisikia hasira zinazidi kuongezeka. Nilitamani nimzabe vibao kama yule Mkuu wa Wilaya aliyemchapa kibao jamaa bila kujali haki za binadamu wala mjukuu wa haki za binadamu. Nilimwangalia kwa jicho la dharau na kebehi. Nilimuongezea na msonyo wa Kichagga.

Alikuwa amevaa shati la mauamaua la rangi nyekundu, kijani, na nyeupe huku akiwa amevaa jeans ya bluu iliyopauka sana. Alikuwa ni kijana kama

wa miaka 28 hivi lakini kwa namna yoyote ile alikuwa chini ya miaka 35. Ukiondoa lafudhi yake hiyo kijana alikuwa ni Rastafariani yaani wale ambao wanaamini katika Mungu wao aitwaye Jah ambao wanamtukuza Mfalme Haile Selassie kama Mungu wao. Dini hiyo ya Marastafari imeenea kwa kiasi kikubwa visiwa vya Jamaika. Nywele zake za kirasta zilikuwa zimefichwa na kofia ya kirasta iliyofumwa ikiwa na rangi za nyekundu, nyeusi, njano na kijani. Zilikuwa zinachungulia kwenye kingo za kofia hiyo kama mashahidi wanaosubiri kutoa ushahidi wa mgongano huo kama. Kwa namna yoyote ile alikuwa ni nadhifu. Alizidi *kunitibua.*

"Acha kunizungumzisha kiingereza chako cha kuokota hapa" niliamua kumtolea uvivu. "Nyinyi ndio mnatakiwa muondoke katikati ya Jiji hapa, mnachafua tu jiji hili na mambo yenu ya kishamba kishamba halafu mnajifanya wasomi" niliamua kuua kabisa!

Wakati huo namfokea huyo kijana Mjamaika uchwara Mzee Yusuph alikuwa ananituliza na kunitaka niachane naye na kumsamehe; watu wengine waliacha shughuli zao na kuniangalia jinsi ambavyo nilikuwa nampaka kijana wa watu. Kwa kweli damu ilikuwa inanichemka na mikono inanitetemeka. Nilipoangalia mkoba wangu mikononi mwa mzee Yusuph niliona umechafuliwa kidogo na ile juisi ingawa nilikuwa na uhakika kuwa nyaraka hazikuchafuliwa. Sasa sijui ndio zingekuwa zimemwagikiwa ingekuwaje. *Watu wengine bwana ushamba mtupu.*

Yule kijana alikuwa kimya, amenyong'onyea na hakutaka kuendelea kusemezana na mimi na taratibu akarudi kuingia kwenye kibanda chake. Alikuwa kama kobe aliyeshtukizwa na kujirudisha gambani kwake au kama

"Au unataka nikupigie mwizi nini ndio utakoma" nilimuuliza kwa hasira. Vijana wengine wakaanza kunisihi kuwa nimsamehe kwani ni kijana mzuri na ni "bahati mbaya" tu. *Mjamaika* yule alikuwa ananiangalia kwa macho ya mshangao na yaliyojaa ishara ya uchungu na maumivu. Sikujali kitu. Niliamua kuondoka hapo nikifuatana na mzee Yusuph. Blauzi yangu nyeupe ilikuwa imechafuliwa kabisa na nilikuwa na uhakika hayo madoa yasingetoka tena. Niliamua hapo hapo kuchepukia upande wa pili wa barabara ambapo kuna maduka ya nguo mbalimbali na sikuchelewa kujipatia blauzi nyingine na kutoka hapo niliingia Wizarani ambako nilitumia muda kubadilisha nguo nikiwa nimekasirika kweli. Sikuelewa kwanini wanaume wengine hawajali kabisa wanavyovifanya kana kwamba havina matokeo yoyote yale.

Niliondoka hapo baada ya kumshukuru mzee Yusuph nikiwahi msongamano wa magari hasa kwenye hiyo barabara yetu ya kwenda Morogoro. Bado nilikuwa na hasira kwanini yule kijana badala ya kuniomba tu msamaha alianza kunizungumzisha kijamaika. Halafu kitendo cha yeye kuondoka na kwenda kibanda chake kilikuwa ni cha dharau sana alitakiwa asimame pale kama mwanamme na kubeba lawama na matusi yote. Kwa kweli nilikuwa na hasira sana.

Nilipofika nyumbani ilikuwa inakaribia saa kumi na mbili za jioni; nimechoka na misuli ya mikono na shingo ilikuwa inaniuma. Ukichanganya na adha ya kuendesha gari kwenye jiji hili tukufu la Lukuvi na mgongano na Mjamaika nilijisikia nimechoka kupita kawaida. Siku yangu ilikuwa inaendelea vizuri hadi yule Mjamaika alipoitibua.

Nilijaza maji kwenye sinki la kuogea na kuweka sabuni ya mapovu ili niweze kujipumzisha kwa muda ndani ya maji hayo yenye uvuguvugu na kupunguza maumivu kwenye viungo mbalimbali vya mwili. Bafu letu liko juu gorofani na limezungukwa na kuta za vioo ambavyo viliruhusu mwangaza kuingia ndani, nje yake kidogo kuna sehemu ya baraza ambapo unaweza kusimama nje au kuweka mojawapo ya vile vitanda kama vya ufukweni na kufurahia jua. Mara kwa mara mchana huwa napumzika hapo. Usiwe na wasiwasi, si rahisi mtu kuona labda apite kwa ndege au helikopta juu. Jioni hiyo miale ya jua lilikuwa likizama lilifanya bafu liwe na rangi ya dhahabu iliyowiva.

Nilichojoa nguo zangu taratibu nikiwa chumbani, nikiuachilia mwili wangu katika utupu wake wa kuzaliwa. Nilivua hereni zangu pamoja na mkufu na bangili na kuviweka kwenye kisanduku cha usalama. Nilijiangalia kwenye kioo wakati napita kuelekea bafuni na nilijipenda. Nilikuwa bado "wamo" na nilijichekelea moyoni jinsi Mungu

alivyonipamba kwa umbile langu. Pamoja na watoto wangu wawili bado niliweza “kumantain figure” yangu vizuri kwa mazoezi ya hapa na pale na kujikeep busy na shughuli mbalimbali. Nilijiangalia nyuma na kuona jinsi ambavyo nilijaliwa. Nikajicheka.

Nilijifunga taulo kichwani kuzuia nywele zangu zisiingie maji. Nilijiteremsha taratibu kwenye sinki hilo mkono wangu wa kulia ukijishikilia kwenye ukuta wa marumaru. Mapovu yaliyofurika yaliupokea mwili wangu kama washangiliaji uwanjani wanavyopokea timu waipendayo. Mwili wangu uliitikia kwa kusisimka kwa kutekenywa na mapovu hayo na ngozi yangu nyororo ikiyasalimu kama rafiki wa zamani. Nilijilaza ndani ya maji hayo nikiachilia kichwa changu tu nje na magoti niliyoyakunja yalijitokeza kama vinara vya Kibo na Mawenzi.

Nilikuwa natumia dodoki la kienyeji kabisa kujisugua taratibu mwili wangu huku nikifurahia utulivu huo ambao niliuhitai kwa siku hiyo. Nilijisikia utulivu na amani ya namna ya pekee na usalama kwani ni katika nyumba yangu nilijihisi niko katika patakatifu; kwenye hekalu ambalo mimi nilikuwa ni kuhani wake mkuu. Nilikuwa nimeweka CD ya marehemu Luther Vandross ya *Forever, For Always for Love* kunisindikiza. Muziki wa gwiji huyo uliniliwaza na kunibembeleza kwa mbali huku ukinikumbusha fungate letu na mme wangu. Tulibahatika kumuona Luther Vandross akiwa ndiyo katika kilele cha kipaji chake. Nilitulia ndani ya maji hayo nikiacha yanitulize na kunifariji, yaniamshe na kunirejeshea utulivu wangu. Nilitaka maji hayo yanikumbatie na yanishikilie yasiniachie. Nilijisikia kama mwali wa miaka kumi na tisa hivi.

Sikutaka kufikiria kitu kingine chochote; sikutaka kufikiria nyumba wala magari, sikutaka kufikiria hoteli wala ofisi. Sikutaka kuwafikiria watoto wala mume. Nilitaka niwe mtupu tu kichwani, nifurahia utulivu huo. Sikutaka kufikiria kitu kingine chochote. Nilijaribu kuwa na ombwe katika fikra zangu. Nilijaribu sana.

Isipokuwa yule kijana aliyenitibua Mjamaika *koko!* Alinishikilia mawazo yangu kama luba; niliweza kuona mgongano wetu ulivyotokea, niliweza kusikia tena mlio wa mkoba wangu kudondoka pembeni na sauti za watu ziking'aka. Nilipokuwa nimefumba macho yangu hivyo huku dodoki nimelishika vyema na kulizungusha kifuani kwangu na kuyasugua matiti yangu, niliweza kuona sura yake yule Mjamaika.

Sikutaka kumfikiria, sikutaka kumuwaza, sikutaka kabisa kumkumbuka. Nilipojaribu kujitahidi kumfuta mjamaika kwenye mawazo yangu wimbo wa Luther wa Once you Know how kwenye hiyo Album uliingia taratibu na kunifanya nianze kufuatisha maneno yake. Nilijisikia donge limekaba; machozi yalianza kunitiririka na pole pole na kwa sauti kama ya kunong'oneza nilimfuata Luther kama mwimbaji msindikizaji.

One day I was cryin'
'Cause I thought that
Love was something that would
Never come my way, no way

That's when somebody told me
Not to worry
They said love would surely one day be my friend
And I would never have to be without it again
And it's because

Chorus:
Once you know how
You just never forget how to
It may seem kinda crazy
But it's a sho-nuff thing
Been tested and found true
Once you know how
You just never forget
How to love

I'm in love
Yes, I am, at last
I can love
Yeah